



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



## HALMASHAURI YA WILAYA MULEBA

*Unapojibu tafadhali taja*

**Kumb. Na.** KGR/MLB/HW/A.225/VOL.V/35

Tarehe: 05/09/2023

### **TANGAZO LA NAFASI YA KAZI (LIMEONGEZWA MUDA WA KUTUMA MAOMBI)**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba anawatangazia nafasi za kazi watanzania wote wenye sifa za kuajiriwa katika nafasi ya Mtendaji wa Kijiji Daraja la III. Hii ni kwa kuzingatia kibali cha Ajira Mbadala chenye Kumb. Na. FA.170/368/01"C"/71 cha tarehe 04/05/2023, na kibali cha Ajira mbadala chenye Kumb. Na. FA.170/368/01"C"/86 cha tarehe 10/07/2023 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Tangazo hili limeongezwa muda wa kutuma maombi kwa lengo la kukidhi takwa la Kanuni za Uendeshaji shughuli za Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma za mwaka 2021, Sura ya 298, kuhusu Tangazo kuwekwa kwenye 'Website' ya Sekretarieti ya Ajira.

Waombaji ambao waliwasilisha maombi yao kwa kuzingatia tangazo lenye Kumb. Na. KGR/MLB/HW/A.225/VOL.V/34 la tarehe 11/8/2023, hawatakiwi kuomba kwa mara nyingine kwa sababu barua zao za maombi zilishapokelewa.

#### **MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III - NAFASI SABA (07)**

##### **SIFA ZA MWOMBAJI**

1. Awe amehitimu Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI).
2. Awe amehitimu mafunzo katika ngazi ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo; Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii, na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

## **KAZI/ MAJUKUMU.**

1. Atakuwa Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji;
2. Atakuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji;
3. Kusimamia Mapato na Matumizi ya Halmashauri ya Kijiji.
4. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji;
5. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji, na Kiongozi wa Wataalamu waliopo katika ngazi ya kijiji.
6. Kutasfiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu za Serikali katika kijiji.
7. Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali;
8. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji;
9. Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji;
10. Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji na
11. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

**Mshahara:** Ngazi ya Mshahara wa Serikali (TGS B).

**Masharti ya Kazi:** Ajira ya Kudumu na Pensheni

## **VIGEZO NA MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI.**

1. Mwombaji awe raia wa Tanzania na umri kuanzia miaka 18 – 45.
2. Mwombaji awe hajawahi kushitakiwa kwa kosa lolote la jinai.
3. Waombaji wote waambatanishe nakala za vyeti vya taaluma, nakala ya cheti cha Kidato cha nne, na sita vilivyothibitishwa na Hakimu au Wakili anayetambulika na Serikali.
4. Waombaji wote waambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
5. Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed Curriculum Vitae) ikiwa na anuani, namba za simu za kuaminika, pamoja na majina

- ya wadhamini (referees) watatu (3) na picha moja ya "passport size" ya hivi karibuni (iandikwe majina kwa nyuma).
6. Testimonials, Provisional Results, Statement of Results, Hati za matokeo za kidato cha nne na sita (Form IV and VI Results Slips) na Transcript ambayo haikuambatanishwa na cheti havitakubaliwa.
  7. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vinahakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (NECTA au NACTE).
  8. Waombaji ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma hawatakiwi kuomba nafasi hizi.
  9. Waombaji watakaowasilisha vyeti, na taarifa za kughushi watachukuliwa hatua za kisheria na mamlaka zinazohusika.
  10. Maombi yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
  11. Kwa waombaji wenye vyeti vya ngazi ya msingi yaani NTA Level 4 (Basic Technician Certificate), na ngazi ya stahhada NTA Level 6, maombi yao hayatahughulikiwa.
  12. Waombaji wote waambatanishe nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA), au Namba ya Utambulisho wa Uraia (National Identification Number) kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
  13. **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 11 Septemba 2023, saa 09:30 Alasiri.**
  14. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kupitia anuani ifuatayo;

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
S. L. P 131,  
MULEBA.**

Dkt. Peter Maiga Nyarja  
**MKURUGENZI MTENDAJI.**

